

UCHAKATAJI WA MIHOGO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Mwezi wa nne mwaka 2018, LIC ilikubaliana na kusaini mkataba na Kibondo Big Power Group (KBPG) kusaidia kumalizia ujenzi wa kiwanda cha kuchakataji na usindikaji wa mihogo ambao ulijumuisha ujenzi wa jengo na kufunga mashine.

KBPG ilianzishwa mnamo mwezi wa saba mwaka 2005 kama kundi la wakulima wilayani Kibondo, mkoa wa Kigoma. Kikundi kilipewa ekari 450 za ardhi na halmashauri ya wilaya. Lengo kuu la kikundi lilikuwa katika mnyororo wa thamani wa zao la muhogo ikiwa ni pamoja na uzalishaji na usindikaji. Kikundi kilikua na wanachama 33 kati ya hao 22 ni wanaume na 13 ni wanawake. Kutokana na changamoto za kiuongozi ndani ya kikundi, mfumo wa kikundi ulirekebishwa na mwanachama mmoja akawa meneja kiuhalisia na wengine kuwa kama wanachama walioajiriwa.



Shamba la mihogo katika KBPG

Mihogo ambayo haijasindikwa/haijachakatwa, Kibondo

Fursa za masoko kwa bidhaa zinazozalishwa na KBPG zinapatikana kote ndani na nchi jirani zikiwemo Burundi, Rwanda, DRC, Uganda na hata Sudani kusini.

Msaada wa LIC kwa KBPG unajumuisha:

- Kumalizia ujenzi wa miundombinu ya vifaa vya usindikaji
- Kununua na kufunga mashine zote za kusindika mihogo ikijumuisha vifaa vya vifungashio
- Ununuzi wa vifaa vya kusambaza maji
- Mfuko wa fedha kwaajili ya kuanzishia kusindika na kutafuta masoko ya unga wa mihogo.



Mashine za kusindika mihogo KPG, Kibondo. Zimefadhiliwa na LIC.

Mafanikio

Msaada unaotolewa na LIC utaimarisha hali ya soko la mihogo na kuleta matokeo chanya kwenye ajira katika mnyororo wa thamani wa zao la muhogo. Uwekezaji wa LIC umetengeneza ajira 20 za kudumu katika kiwanda cha usindikaji mihogo na kinatarajiwa kusaidia vibarua 90 wanaoajiriwa kila kipindi cha mavuno kupitia KBPG pekee. Kulingana ya hali ya soko la muhogo baadae, kiwanda kitaweza kuongeza uzalishaji na kuchukua zao la mihogo kutoka kwa wakulima wadogo katika eneo hilo.

Ongezeko la thamani kwa zao la muhogo litafungua fursa mpya kwa wazalishaji wa ndani wa zao hilo na kuhamasisha wawekezaji kujiunga na mnyonyoro wa thamani. Kwa sasa usafirishwaji wa zao la mihogo nje ya mkoa wa Kigoma kwa kiasi kikubwa linafanyika kwa mihogo ghafi, iliyokaushwa yenye bei ndogo. Wakulima wa mihogo mkoani humo bado hawajafika kwenye ngazi ya masoko ya thamani ya juu na bidhaa zenye kukidhi viwango. Ushirikiano kufikia lengo hilo umeanzishwa na kampuni ya kichina na njia nyingine ili kufikia uhitaji wa soko wa kuzalisha bidhaa bora zimekuwa zikifanywa na KBPG.

Elimu na kituo cha mafunzo:

KBPG inatoa mafunzo ya kilimo na usindikaji wa mihogo kwa wakulima wa ndani na wa wilaya za jirani. Mbali na hayo, KBPG iko katika mchakato wa kusaidia programu ya mafunzo kwa vijana itakayolenga si tu mihogo lakini pia mazao mengine kama ndizi, na miti ya matunda. KBPG pia itafanya ufugaji wa nyuki ambao utajumuishwa kwenye programu ya mafunzo. Mpango huu wa programu ya vijana una uwezekano mkubwa wa kupata msaada kutoka LIC, ambao utanzishwa na kutekelezwa kwa kushirikiana na halmashauri ya wilaya ya Kibondo na Kibondo Folk Development Centre (FDC). Baadhi ya malazi na vifaa vya mafunzo vitaanzishwa na KBPG pamoja na halmashauri ya wilaya ya Kibondo huku FDC itasaidia kuandaa mtaala na kutoa walimu /wakufunzi.

Moja ya funzo kuu kutoka kwenye mradi wa LIC lipo kwenye suala zima la menejimenti. Changamoto za kusimamia uzalishaji katika hatua za awali na usindikaji kupitia kamati ya kikundi kuna athiri ufanisi na uzalishaji kwa kiasi kikubwa. Usimamizi mzuri ndio nguzo kuu ya mafanikio. LIC pamoja na washirika wake wameendelea kutafuta njia mbalimbali za kupata chombo bora kitakachosimamia kwa ufanisi miradi ya uwekezaji wa pamoja kati serikali na sekta binafsi na uwekezaji wa taasisi za wakulima/wazalishaji.

Mradi wa **LIC** umewekeza kiasi cha shilingi milioni 26 katika kiwanda cha kusindika mihogo cha Kibondo Big Power Group.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya mradi wa LIC: www.lic.or.tz